

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



WIZARA YA AFYA

TAARIFA KWA UMMA

**MWENENDO WA UVIKO-19 KWA KIPINDI CHA TAREHE 27 AGOSTI HADI 07
OKTOBA, 2022**

DODOMA: 08 Oktoba, 2022

Ndugu Wananchi, Serikali kupitia Wizara ya Afya, imeendelea kuimarisha mapambano dhidi ya UVIKO-19 nchini na inaendelea kutoa taarifa kwa umma kuhusu mwenendo wa ugonjwa huu. Katika kipindi cha tarehe **26 Agosti hadi 07 Oktoba, 2022**, jumla ya visa vipyta **478** vimethibitika kuwa na maambukizi ya UVIKO – 19 ikilinganishwa na visa **586** kwa kipindi cha mwezi mmoja uliopita kuanzia tarehe 30 Julai hadi 26 Agosti 2022, ambalo ni punguko la asilimia **18.4**. Aidha, katika kipindi hicho, hakukuwa na vifo ukilinganisha na kipindi cha tarehe 30 Julai - 26 Agosti 2022 ambapo kulikuwa na vifo **4** vilivyoripotiwa kutokana na UVIKO-19.

Ndugu Wananchi, Mchanganuo wa takwimu katika kipindi cha tarehe 27 Agosti hadi 07 Oktoba, 2022 unaonesha kuwa, watu waliothibitika kuwa na ugonjwa huo walitoka katika Mikoa 17 ikiwemo; Dar es Salaam (**382**), Mwanza (**28**), Arusha (**23**), Mara (**8**), Dodoma (**5**), Manyara (**5**), Morogoro (**5**), Lindi (**4**), Mbeya (**4**), Singida (**3**), Pwani (**2**), Kigoma (**2**), Katavi (**2**), Ruvuma (**2**), Mtwara (**1**), Kilimanjaro (**1**) na Tanga (**1**). Aidha, jumla ya wagonjwa wanne (**4**) waliothibitika kuwa na UVIKO-19 walilazwa na wote walikuwa hawajapata chanjo ikiwa ni punguko la wagonjwa wanne ukilinganisha na wagonjwa **8** walitolewa tarifa kwenye tamko liliopita.

Ndugu Wananchi, Serikali imeendelea kutoa huduma za chanjo ya UVIKO-19 nchini ili kuwawezesha wananchi kupata kinga dhidi ya ugonjwa huu. Kuanzia tarehe **27 Agosti**


hadi 07 Oktoba, 2022 jumla ya Wananchi wenyе umri wa miaka 18 na kuendelea waliopata dozi kamili ya chanjo ya UVIKO-19 walikuwa **3,499,099** ambapo ni punguko la asilimia **10.3** ukilinganisha na watu **3,902,839** waliopata dozi kamili katika wiki ya tarehe 30 Julai - 26 Agosti 2022.

Ndugu Wananchi, Tangu chanjo za UVIKO zimeanza kutolea mpaka kufikia tarehe 07 Oktoba 2022 jumla ya Wananchi waliopata dozi kamili ni **22,098,872** kati ya watu **30,740,928 (71.89%)**. Lengo ni kuchanja 100% ya Watanzania wote wenyе umri wa miaka 18 na kuendelea. Aidha, Wizara inaendelea kuwahimiza wananchi kupata na kukamilisha dozi za chanjo ya UVIKO-19 ili kuzuia kupata ugonjwa mkali hata kifo, pale mtu anapopata maambukizi.

Ndugu Wananchi, Wizara inatoa tahadhari kwa wananchi wote kuendelea kuchukua hatua za kujikinga na UVIKO – 19 ikiwa ni pamoja na:

- Kupata kwa wakati dozi kamili za chanjo ya UVIKO - 19
- Kuvalaa barakoa pindi unapojisikia dalili za mafua ili kuzuia kusambaa kwa maambukizi.
- Kuzingatia usafi binafsi ikiwemo kunawa mikono mara kwa mara kwa maji tiririka na sabuni au kutumia vipukusi (sanitizer).
- Kuwahi kwenye vituo vya kutolea huduma za afya endapo utakuwa na dalili za ugonjwa huu
- Kuendelea kuchukua hatua za kujenga mwili kwa kufanya mazoezi na kula vyakula bora
- Kutoa taarifa za kuwepo watu wenyе dalili za ugonjwa huu katika jamii kuitia namba ya simu ya bure **199**.

Imetolewa na:



Dkt. Aifello W. Sichalwe
MGANGA MKUU WA SERIKALI